

# Upandaji wa Miti - Afforestation

## KITALU CHA MITI

Ni eneo lilotengwa kwa ajili kuzalisha na kutunza miche ya miti kabla ya kupelekwa shambani na kupandwa kwa matumizi mbali mbali.

## TREE NURSERY

*A tree nursery can be defined as a piece of land prepared for raising tree seedlings to be carefully maintained up to a stage that the young material is able to establish and finish under field condition.*

## Jinsi ya kuanzisha kitalu cha miti

Kabla hujaanzisha kitalu cha miti ni lazima kuzingatia yafuatayo:

- Kuwa na mpango dhabiti wa utekelezaji kuanzia gharama zitakazotumika wakati wa utekelezaji hadi usambazaji
- Kuweka malengo ya uzalishaji. Ni lazima kujua idadi ya miti itakayozalishwa ili kuweza kutathimini kiwango cha mafanikio.
- Utunzaji na muda. Wakati wa kuanzisha kitalu cha miti unaweza ukafupisha au kuongeza muda wa utunzaji kulingana na aina ya miti (miti inayokua haraka na ile inayokua polepole).
- Nimuhimu kufahamu muda wa mbegu kuota na kukua kabla ya kuanzisha kitalu cha miti.
- Ratiba ya kazi. Wahusika lazima wafahamu kazi zile ambazo hufanyika kila siku na zile ambazo hufanyika baada ya muda. Mafano;- Unywesheaji wa mara kwa mara, ukataji/upunguzaji mizizi n.k.
- Aina ya kitalu. Kitalu kikubwa kinachohitaji vibarua, kikundi au mtu binafsi.

## How to start a tree nursery?

*Before starting a tree nursery consider the following:-*

- *Planning and operation - These include all aspects of budgeting to distribution*
- *Setting targets for production - A number of tree seedling to be produce should be known to enable the evaluate of the achievement in terms of number and percentage. Setting of targets should be equivalent to the demand and supply.*
- *Management and time - Time for the establishment of a tree nursery can shorten the period for management (fast growing spp) or prolong (low growing spp). Management of a tree nursery starts from seed bed to the transplant bed to planting out. Therefore, it is very important to know the germination period of every individual tree spp. In addition, growth rates before establishing a tree nursery.*
- *Work schedule - The actors should know the necessary duties to be performed daily or after a certain stage. (e.g. regular watering, root pruning etc.)*
- *Type of nursery - Central, group or individual (home stead) tree nursery*

## Masharti

- Kiwe karibu na eneo lenye maji ya kudumu
- Penye kivuli - chini ya mti au chini ya kichanja
- Sehemu ambayo haiwezi kufikiwa na wanyama (unaweza kutengeneza uzio)
- Pawepo na mwinuko wa kadri (sehemu zenye mteremko mkali matuta ya ngazi yatasaidia)
- Karibu na nyenzo (mfano, mchanga,

udongo wa msituni/pori-unaweza kupatikana chini ya miti mikubwa na vichakani)

- Pia ni vizuri kiwe karibu na shamba ili kurahisisha upandaji na kupunguza gharama ya usafirishaji
- Kiwe katika eneo linalopitika wakati wowote

### **Conditions**

- *Near permanent source of water.*
- *Shade - this can be under the large tree or creating an artificial shade.*
- *Protected from livestock - this can be done by fencing e.g. with local available thorn bush.*
- *As level as possible (gentle slope) and well drained soil - for steep areas this can be achieved by terracing.*
- *Near adequate supply of ingredients materials - e.g. sand, forest soil (can be obtained from bush or under big tree etc.).*
- *Preferably near the planting site - This can ease the planting operation and thus reduce the transplant costs.*
- *Accessibility*

### **Faida ya kitalu cha miti**

- Kupanda miti unayoipenda
- Upatikanaji wa miche kwa urahisi na kwa wakati
- Hakihitaji gharama kubwa kikianzishwa kwenye makazi.
- Hutumia rasilmali asili (majani ya migomba, makopo nk.)
- Huongeza kipato kwa kuuza miche ya

ziada

- Huendeleza upandaji wa miti
- Utaalamu wa jamii

### **Advantages of tree nursery**


- *Able to plant trees according to your priority.*
- *Available to tree seedling at right time*
- *Not necessarily, require high cost if established at home stead level or groups.*
- *Make use of the available local resources*
- *Income regenerating*
- *Speed up the afforestation process.*
- *Community capacity building.*

### **Faida ya upandaji miti**

- Huzuia upepo.
- Huongeza mboji kwa njia ya majani
- Husaidia kuvuta mvua
- Hubadilisha hali ya hewa (kivuli)
- Mizizi hushika ardhi hivyo kuzuia mmomonyoko
- Hewa safi
- Hutupatia mbao, kuni, madawa, fito za kujengea nk.

### **Advantages of tree planting**

- *Wind break.*
- *Improve the soil organic matter.*
- *Encourage the availability of rain.*
- *Provides shade and suitable environment to live.*
- *Controls soil erosion due to its root system*
- *Provides oxygen*
- *Provides timber, fuel wood, medicine, building material etc.*



### **Traditional Irrigation & Environmental Development Organization**

PO Box 8909, Moshi – Tanzania

Telephone: +255 27 27 273025 / 2754232

Email: [tip@tiptz.org](mailto:tip@tiptz.org) Web: [www.tiptz.org](http://www.tiptz.org)